



Kuunganisha Familia zilizo na Watoto katika Pre-K hadi Gredi ya 12 katika Philadelphia na Intaneti ya Bila Malipo au Gharama Nafuu

Mafunzo hayaishi unapoondoka darasani.

Je, PHLConnectED ni nini?

PHLConnectED ni mradi wa Jiji wa kuzisaidia familia zilizo na wanafunzi katika Pre-K hadi Gredi ya 12 kufikia intaneti ya bila malipo au ya gharama nafuu.

Je, mradi wa PHLConnectED unasaidia familia kwa njia gani?

Familia zinaweza kupata usaidizi binafsi kutoka kwa Msaidizi wa Dijitali wa PHLConnectED ili:

- kukagua chaguo zinazopatikana za intaneti ya bila malipo au gharama nafuu.
- kusaidiwa kufikia na kutumia teknolojia.
- kufikia madarasa na nyenzo za ujuzi wa kidijitali kote katika Philadelphia.

Jinsi ya Kuunganishwa

Ili upate maelezo zaidi, **piga simu kwa 2-1-1**. Kwa huduma za usaidizi wa lugha, **bonyeza 8**.

Simu hii ya dharura inapatikana saa 24 kwa siku, siku 7 kwa wiki na inatoa huduma kwa zaidi ya lugha 150.

Je, nani anaweza kuunganishwa kupitia mradi wa PHLConnectED?

Familia zinaweza kustahiki kuunganishwa na mtandaopepe wa T-mobile wa PHLConnectED ikiwa:

- Zina mtoto katika PreK hadi Gredi ya 12 aliyeandikishwa katika shule ya Philadelphia
- Hazina ufikiaji wa intaneti ya kebo nyumbani, zinaweza tu kufikia intaneti kupitia kifaa cha mkononi, au hazina makazi au ziko katika makazi ya muda
- Zinashiriki katika mipango fulani ya msaada wa serikali kwa kutimiza masharti ya mapato